

Polisi ndani ya tope la kashfa

● Wadaiwa kuua mtuhumiwa na baadaye kumzamisha ziwani

soma
Uk. 4



Soma Ndani

TPA yawapa siri wafanyabiashara



Na Mwandishi WETU

WAFANYABIASHARA wanaoagiza bidhaa kutoka nje ya Tanzania, wamepewa siri ya kutengeneza faida kubwa kwenye shughuli zao; kuwa ni kutumia meli kubwa kuleta mizigo yao.

Soma zaidi Uk. 16

Madeni ya wakandarasi yatisha Bunge

Soma zaidi Uk. 25

Uchunguzi

Hatua kwa hatua alivyotekwa, kuuawa Asiimwe

SIKU chache baada ya kuibuka kwa taarifa za tukio la kushtua la kutekwa kwa binti mwenye ualibino **zaidi Uk. 6**



Mtoto Asiimwe na baba yake

Safu kamambe

- Askofu Bagonza
- Evarist Chahali
- Jerry Muro
- Jicho la Tai

Tahariri/Katuni

Hata shetani anatushangaa kuua albino

NCHINI Tanzania kuna albino mmoja katika kila watoto 1429 wanaozaliwa. Miongoni mwa Watoto hawa ni mtoto aitwaye Asiimwe Novart.

Asiimwe alitekwa nyumbani kwao Mei 30, mwaka huu, na siku 19 baadaye mwili wake ukaokotwa, baadhi ya viungo vya mwili wake vikiwa vimekatwa.

Binti huyo huenda asiwe mwisho kuua-wa, kwai mauaji ya albino yamekuwa ya kiibuka, hasa kwenye misimu ya kila uchaguzi kutokana na imani za kishirikina kuwa viungo vya mwili wa albino huleta bahati, utajiri na ushindi.

Hivyo, bado baadhi ya Watanzania wanafikiri, kuhukumu na kutenda kutokana na sababu za kishirikina, badala ya sababu za kisayansi.

Kifikra, sayansi imekuwa chachu yenye nguvu za kuyeyusha chembechembe za imani za kimapokeo ambazo ni kinyume na ukweli halisi.

Mfano, sayansi imeyeyusha mapokeo yafuatayo; kwamba maradhi hutokana na uchawi; mavuno hafifu shambani hutokana na hasira za miungu au pepo wabaya na au kuwatoa kafara watu ni sababu ya ushindi vitani.

Kamwe viungo vya albino haviwezi kuwa chimbuko la ushindi wa kisiasa, kama ambavyo imani haba haziwezi kuwa sababu ya mkate kubadilika kuwa mwili wa mtu.

Sisi Pambazuko tunaamini kuwa ni ujinga wa watu wetu wengi ndiyo imekuwa sababu ya kukumbatia ushirikina unaosababisha kudanganywa na waganga kwamba kuua binadamu ni chanzo cha mafanikio badala ya kufanya kazi kwa bidii na maarifa.

Mbali na kufanya kazi kwa bidii, pia inaonekana elimu ya watu wengi iliyopatikana darasani, bado haisaidii, kiasi kwamba wanayofanya vitendo vya mauaji, huenda hata shetani, tunayemlaani kwa kila jambo baya, anatushangaa Watanzania.



Kidijitali zaidi!



Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa Tanzania, January Makamba akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika (AU-PSC)- ngazi ya wakuu wa nchi, uliofanyika kwa njia ya mtandao, kujadili hali ya usalama nchini Sudan. Mkutano huo ulifanyika juzi - Jumamosi, Juni 21. (Picha kutoka Mtandao wa X).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Mkurugenzi anakula rushwa, anaiba uchaguzi kumsaidia mbunge au diwani, baada ya ushindi wa hao viongozi na kuanza kazi, mkurugenzi anabainika kula rushwa, kisha waliokula rushwa kushinda, wanajitokeza kukemea. Mkurugenzi anashangaa! – Godbless Lema.

Habari

Polisi ndani ya tope la kashfa

● Wadaiwa kuua mtuhumiwa na kumzamisha ziwani



Marehemu Baraka

Na Waandishi WETU

JESHI la Polisi limeingia katika kashfa nzito likihusishwa na mauaji ya mtuhumiwa aliye-shikiliwa Kituo cha Polisi, ambaye mwili wake - usio na uhai, ulikutwa umefungwa jiwe na kuzamishwa Ziwa Victoria.

Uchunguzi wa gazeti la Pambazuko umebaini kuwa kabla ya kupotea 'kiutatanishi,' mtu huyo alikuwa akishikiliwa katika Kituo Kido-go cha Polisi cha Kisiwa cha Goziba, Wilaya ya Muleba, Kagera.

Gazeti hili limeelezwa kuwa mtuhumiwa huyo, Baraka Lucas (23) alikamatwa na kupele-

kwa kituoni hapo Jumapili – Juni 9 na alipotea akiwa bado anashikiliwa na Polisi kituoni hapo Juni 11.

Baada ya siku nne za kutofahamika alipo, mwili wa Baraka ulipatikana Jumamosi - Juni 15, huku mikono yake ikiwa imefungwa kamba.

Ndugu wa marehemu aliyejitambulisha kwa Pambazuko kwa jina la Paschal Ibrahim, amesema kwamba Baraka, aliyekuwa akijishughulisha na kazi ya kusomba dagaa kisiwani hapo, alikamatwa na askari polisi wa kituo hicho kwa madai ya kuwa mzururaji.

Imebainika kuwa kundi la askari polisi wa kituo hicho walimkamata Baraka majira ya usiku akiwa na wenzake wakati walipokuwa katika matembezi yao ya kawaida.

“Hapa kisiwani kwetu kuna tukio baya sana limetokea ambapo ndugu yangu aitwaye Baraka, alipotea akiwa mikononi mwa polisi, kisha mwili wake kuokotwa katika Ziwa Victoria ukiwa unaelea majini huku kukiwa na mazingira kwamba mwili huo ulikuwa umezamishwa kwa kufungwa jiwe...

“Baraka alikamatwa na rafiki yake maarufu kwa jina la Yolo wakati wakiwa katika matembezi yao ya kawaida usiku na kupelekwa kituo cha Polisi ambako walishikiliwa kwa muda wote wawili na baadaye Yolo alifanikiwa kutoka, lakini Baraka akaendelea kushikiliwa kwa kosa hilo-hilo la uzembe na uzururaji...

“Wakati wote Baraka alipokuwa kituoni hapo, mimi nilikuwa nikimpelekea chakula, lakini jana asubuhi (Juni 12, mwaka huu), nilipopeleka chakula, polisi waliniambia Baraka hakuwapo kituoni hapo kwa sababu alikuwa amedhaminiwa na rafiki yake wa kike...

“Waliponiambia hivyo, nikawauliza huyo aliyemdhamini ndugu yangu ni nani kwa sababu hana historia ya kuwa na mpenzi hapa kisiwani...

Inaendelea Uk. 15

‘Comeback’ ya Mbowe, Lissu yafurahiwa

Na Igo AI

VIONGOZI wa juu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), wametangaza kwamba wameanza “mchakamchaka” wa pamoja wa kukiamsha chama chao, hasa mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

Kwamba viongozi hao wa juu; mwenyekiti Freeman Mbowe na makamu wake, Tundu Lissu, kuanza kufanya kazi pamoja, kusafiri pamoja, kuzungumza lugha moja wanapokuwa majukwani, ni hatua ambayo imemfurahisha zaidi Mzee Tai.

Kutokana na kuhuishwa kwa uhusiano wa viongozi hao wa juu wa chama kikubwa cha upinzani cha Chadema, Mzee Tai ameamua “kujianika” – bila kuogopa, kupongeza na anadai kuwa anafanya hivyo kwa maslahi ya Tanzania.

Ikumbukwe kuwa Mzee Tai ni shabiki nambari wani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kile chama tawala, ambacho anaamini kuwa “kitaongoza na kutawala milele Tanzania.”

Mzee Tai pamoja na kuwa kada, bado anaamini kuwa upinzani imara ndiyo unakiimarisha chama chake na kumpa mwenyekiti wake, Rais Samia Suluhu Hassan, munkari wa kufanya kazi zaidi kwa manufaa ya Watanzania.

Sinia sitizeni huyo anadai kuwa haku-na mwana-CCM makini anayetamani upinzani ufe, kwani ikitokea hivyo, basi chama hicho tawala na viongozi wake watajiona miungu watu na kwamba hawatawatendea vyema wananchi.

Akizungumza na waandishi wa

habari, Mzee Tai amesema atapandwa na hasira ikiwa kutatokea mwanachama mwenzake wa CCM, akazuia maandamano ama mikutano ya Chadema, kwani kwa kufanya hivyo, atakuwa ni ama mnafiki au mtu wa kujipendekeza; eti lazima atakuwa “chawa au anautafuta ujinga huo.”

“Napenda kuona hawa Chadema, wakiandamana, wakijenga hoja zao vyema, haya mambo tulikaribia kuyakosa kwa kuwa Mbowe na Lissu, walikuwa wakielekea machinjioni, kwamba almanusura kuachana kwa kuwa tu kulikuwa na mdudu kati yao,” amesema Mzee Tai, bila kumtaja huyo mdudu ni nani.



Green Horizon
Mowing & LawnCare

GO GREEN
GO CLEAN

Save 20% on your first booking with us!

OUR SERVICES

- Domestic and Outside Maintenances
- Garden,
- Mowing and lawn care,
- Pressure Washing
- Tree and hedge trimming
- Landscaping Design
- Garden Renovation

HELPING TO KEEP OUR COMMUNITY CLEAN

0713-821 441
0672-782 223

Makongo CCM

Mowinandlawn_care

Habari

Hatua kwa hatua Asiimwe alivyotekwa, kuuawa

Na Waandishi WETU, Muleba

SIKU chache baada ya kuibuka kwa taarifa za tukio la kushtua la kutekwa kwa binti mwenye ualibino, Asiimwe Novart (miaka miwili na nusu) huko Bukoba, Pambazuko lilipiga kambi eneo hilo ili kupata mtiririko wa taarifa za kina na sahihi kuhusiana na tukio hilo.

Kazi ya kupata ukweli wa tukio lenyewe ilidumu kwa siku sita ambapo gazeti hili limezungumza na kufanya mawasiliano na watu mbalimbali kuhusiana na tukio hilo.

Yaliyojiri yameelezwa ndani ya Pambazuko, huku mtandao wa kumuua Asiimwe ukiwekwa bayana kwa kuwahusisha ndugu wa karibu, akiwamo baba wa binti huyo

Uchunguzi huo unaleta matokeo ya siyokuwa na chembe ya shaka na kwamba Pambazuko liko kazini kufuatilia na kuibua yale ambayo hayaelezwili na chombo kingine cha habari.

Ni kutokana na uchunguzi huo, sasa jamii na dunia itaelewa hatua kwa hatua; tangu mipango ya kumpata Asiimwe ilivyofanyika, kutekwa kwake hadi harakati za kiuchunguzi za Polisi zilivyowezesha kukamatwa kwa watuhumiwa tisa akiwamo baba mzazi wa binti huyo, Novart Venant na padre wa Kanisa Katoliki, Elipidius Rwegoshora.

Kutokana na hofu ya kuhusishwa na kesi hii nyeti wengi wa walioongea na Pambazuko walifanya hivyo kwa sharti la kutotajwa gazetini.

Maisha ya Asiimwe

Mwenyekiti wa Kijiji cha Bulamula, Domesian Rushongama, alieleza Pambazuko kuwa Asiimwe alikuwa akiishi maisha ya kawaida ya watoto wadogo pamoja na wazazi wake katika kitongoji cha Mbale katika kijiji hicho.

Anasema kuwa licha ya kuwa na ulemavu wa ngozi, Asiimwe alikuwa ni binti aliyeishi maisha ya kawaida katika



Mtoto Asiimwe

familia masikini kijijini.

Kebyera Richard, mama mzazi wa mtoto Asiimwe, alimlea mtoto wake kama ambavyo akina mama wengine katika maeneo ya vijijini wanawalea watoto wao, lakini kutokana na hali yake ya ualbino alihakikisha mara nyingi anakuwa naye kwenye shughuli zake kama njia ya kumlinda.

Akiwa katika mazingira ya nyumbani Asiimwe alikuwa akijichanganya na kucheza na watoto wenzake ambao wanaishi jirani na kwao.

Njama za utekaji wa Asiimwe

Mtoto Asiimwe alitekwa na vijana wawili usiku wa Mei 30, mwaka huu katika Kijiji cha Bulamula, Kata ya Kamachumu, Wilaya ya Muleba mkoani Kagera.

Pambazuko limebaini kuwa saa chache kabla ya utekeji huo, baba mzazi wa Asiimwe, ambaye ni dereva wa boda boda, alimpigia simu mke wake, ambaye alikua kwa rafiki yake anayefanya biashara ndogo ndogo katika eneo maarufu la biashara lijulikanalo kama Makutano katika kijiji cha Mbale, akimtaka afunge biashara zake ili arejee nyumbani amtararishie chakula.

Baada ya kupokea agizo la mume wake majira hayo ya jioni, mama Asiimwe alimuuliza mumewe kwa nini asimpitie ili warejee wote nyumbani – kwa kuwa alikuwa

Inatoka Uk. 6

bado kazini, lakini mumewe huyo alisisitiza kuwa mkewe atangulie kuandaa chai na yeye anakuja na sukari, ili baadaye apike chakula kikuu.

Mama Asimwe aliamua kutii agizo la mumewe, alimuaga rafiki yake kuwa anarejea nyumbani kwenenda kumuandalia mume wake chai.

Alipofika nyumbani, alianza kuandaa chai ya mumewe, lakini hadi giza linaingia, mumewe huyo hakuwa amerejea.

Ilipokaribia majira ya saa mbili, alisikia sauti ya kijana nje ya nyumba akiomba msaada wa chumvi ili aitumie kujitibu baada ya kugongwa na nyoka.

Kwa moyo wake wa huruma, na kwa dhamira ya kutoa msaada, kwa haraka mama Asimwe aliacha kazi zake ndani na kukimbilia nje huku akiwa na chumvi hiyo.

Lakini, alipofika nje, alijikuta akikabwa na mmoja wa vijana hao na kumziba mdomo, jambo lililomfanya ashindwe kupiga kelele za kuomba msaada.

Wakati huo, kijana mwingine aliingia ndani ya nyumba na kumbeba kwa nguvu Asimwe, ambaye hakujua kilichokuwa kinaendelea.

Ilibainika baadaye kuwa kulikuwa na vijana wawili ambao baada ya kumchukua Asimwe, walitokomea kwenye migomba wakiwa wamemteka binti huyo na kumwacha mama yake akiwa katika hali ya kuzirai.



Baba yake Asimwe - Novart Venant.

Hatua kwa hatua Asimwe alivyotekwa, kuuawa

Alipozinduka, mama huyo alipiga yowe na majirani walikusanyika na akawasimulia kili-chotokea.

Mara moja msako wa kuwapata watu hao ulianza katika maeneo ya karibu, lakini giza lilikuwa limetanda – kwani ilikuwa imetimu majira ya saa tatu usiku.

“Kama unavyoona, eneo lina migomba tele, nyumba imezungukwa na migomba na kutokana na giza ilikuwa vigumu sana kufuatilia vijana hao walipotorokea na mtoto,” anasimulia mmoja wa majirani.

Hadi wakati huo baba wa mtoto huyo hakuwa amerejea nyumbani licha ya kutoa taarifa kwa mkewe awali kuwa alitaka aandaliwe chai haraka.

Baba Asimwe alipigiwa simu baada ya watu kukusanyika, lakini haikupatikana na ilikuwa ikieleza ujumbe kutoka kampuni ya simu kuwa “namba unayopiga haipatikani kwa sasa...”

Majirani waliendelea na msako maeneo ya jirani na wengine wakakusanyika nyumbani kwa mama huyo, wakijadiliana kuhusu nini cha kufanya.

“Hadi wakati huo tulishangaa baba wa mtoto yuko wapi wakati alikuwa ametoa taarifa kwa mkewe mapema kuwa anarejea kuja kula, na kuwa achemshiwe chai kwanza haraka,” anasema jirani mwingine.

Baba wa Asimwe alifika nyumbani majira ya saa tisa usiku na alipohojiwa alikuwa wapi, alisema alikuwa amempeleka abiria eneo la Kama-chumu Centre, ambako ni mbali na nyumbani.

“Hilo lilituacha na mshangao kidogo maana kwa kawaida katika eneo letu hili halina abiria wa kusafiri usiku wa manane namna hiyo,” anaongeza jirani huyo.

Lakini, naye aliungana na majirani akishangaa kwa lililotokea katika familia yake.

Baada ya muda kidogo, baba huyo alisikika

Inaendelea Uk. 8

Habari

Hatua kwa hatua Asiimwe alivyotekwa, kuuawa



Padre Elipidius Rwegoshora.

Inatoka Uk. 7

akisema kuwa ameokota simu ya mke wake ambayo ilipotea wakati wa kurupushani na vijana wale wawili.

Usiku huo, vyombo vya habari vilipewa taarifa na askari polisi walifika asubuhi yake na kuungana na “wananzengo” katika msako wa binti huyo.

Baada ya hapo polisi hawakutoa taarifa ya kili-choendelea kwa muda wa takribani wiki mbili kabla ya kutoa taarifa kwa umma kuelezea kukamatwa kwa watuhumiwa wengine.

Baada ya msako mkubwa uliofanywa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kagera, Juni 19, 2024, zaidi ya wiki mbili baada ya tukio la kutekwa kwa mtoto Asiimwe, walikamatwa watu wanane, akiwemo baba mzazi wa Asiimwe kwa tuhuma za kuhusika na tukio hilo.

Pamoja na mambo mengine, majirani waliozungumza na Pambazuko walieleza kuwa baba wa mtoto huyo alianza kuhisiwa kuhusika na tukio hilo kutokana na kauli ambazo alikuwa amezitoa siku za nyuma baada ya kuzaliwa kwa Asiimwe.

Mama wa Asiimwe alishawahi kuwadokeza majirani zake kuwa mumewe alikuwa amemkataa mtoto huyo akidai kuwa yeye hawezi kuzaa mtoto mwenye ualbino.

Aidha, mazingira ya siku ya tukio yaliwafanya watu waanze kumhusisha na tukio hilo wakihoji kilichomchelewesha kurudi nyumbani, licha ya kutoa agizo kuwa aandaliwe chai kwani alikuwa njiani akirejea nyumbani.

Mmoja wa majirani aliyezungumza na Pambazuko kwa sharti la kutotajwa jina lake gazetini alisema “mazingira yote ya kutofika nyumbani mapema kwa baba Asiimwe yanatia shaka.

“Kinachoshangaza ni kuwa pamoja na kwamba baba Asiimwe, ambaye alikuwa anamsisitiza mkewe kufunga biashara na kurudi nyumbani tangu saa moja usiku, hakuonekana na simu yake ilikuwa haipatikani...

“Baada ya wananchi kukusanyika hapa nyumbani na kuanza msako baada ya mtoto kutekwa, licha ya kumpigia simu lakini hakupatikana. Alirudi hapa majira ya saa tisa usiku akiwa hana maelezo ya kueleweka alikuwa wapi muda wote huo,” alieleza kwa masikitiko.

Aliongeza; “pia tuna mashaka ya upatikanaji wa simu ya mkewe maana muda mrefu watu walikuwa wamekaa katika eneo lile, lakini hakuna aliyeiona simu. Ilikuware yeye ndiye aliiona ghafala?”

Jirani huyo anasema minong’ono ya baba Asiimwe kuhusika siku kadhaa kabla ya siku ya utekaji na baadaye vyombo vya dola vilipotoa taarifa ya kumhusisha na tukio la mwanaye, ndipo watu wameanza kuunganisha nukta za maneno yake.

Wanasema pamoja na kumkana mtoto huyo, lakini katika siku za hivi karibuni baba Asiimwe alikuwa akijinadi kwa watu kuwa hivi karibuni atapata fedha nyingi zitakazomwezesha kununua pikipiki yake na ataachana na pikipiki za kukodishwa kwa mikataba.

Mbali na hilo, watu walio karibu na mama Asiimwe, walidai kuwa kwa muda mrefu wana-

Inaendelea Uk. 9

Hatua kwa hatua Asiimwe alivyotekwa, kuuawa

Inatoka Uk. 8

ndoa hao walikuwa na ugomvi wa chini chini kuhusu kuzaa mtoto mwenye ualbino.

“Mara nyingi mama Asiimwe alikuwa akilalamika kuwa mumewe anamsumbua mara kwa mara akimlaumu kuwa kwao hakuna mwenye ualbino, hivyo amtafute baba wa mtoto huyo,” alidai jirani huyo.

Eneo ambalo baba Asiimwe alikuwa akiishi na familia yake katika kijiji cha Mbale, eneo lilalomilikiwa na mama yake. Kijana huyo ni wa asili ya kijiji cha Bushagara ambako ndiko pia anakotoka Padre anayetuhumiwa katika mauaji hayo.

Ukamataji

Baada ya kupokea taarifa za utekaji huo, Jeshi la Polisi liliendesha operesheni ya usiku na mchana kuhakikisha wahalifu hao wanakamatwa.

Mashuhuda walioshuhudia ukamataji huo usiku wa kuamkia Juni 19, 2024, walisema ilikuwa kama vita katika Kijiji cha Nyakahama ambapo watu zaidi ya wanne akiwemo mganga wa kienyeji, walikamatwa majira ya saa saba usiku.

“Kundi la watu wakiwa na magari na silaha nzito lilifika eneo hilo na kuanza msako wa nyumba kwa nyumba... ilikuwa ni taharuki kubwa, wananchi waliingia hofu na kudai majambazi wamevamia kijiji, kumbe walikuwa askari wa vyombo vya ulinzi na usalama,” alisema shuhuda mwingine.

Kwa mujibu wa taarifa ambazo Pambazuko imezikusanya, baada ya kukamatwa kwa baba Asiimwe, polisi walimbana na hatimaye alikiri kuhusika na tukio hilo na kisha kuwataja alio Shirikiana nao.

Baada ya baba Asiimwe kutoa maelezo hayo, polisi walianza kufuatilia nyendo za watu walio tajwa, wakitumia njia za intelijensia ya kufuatilia mawasiliano kwa njia ya simu za mikononi na ndipo mtandao huo ulipogundulika na kuwezesha kuwakamata watu wengine watano akiwamo padre wa Kanisa Katoliki, Elipidius Rwegoshora, aliyekuwa anahudumu katika Parokia ya Bugandika.

Hata hivyo inaelezwa kuwa Padre huyu haku

wa anaishi Parokiani hapo, alikuwa akiishi kijijini kwao Bushagara na kuja parokiani hapo na akimaliza huduma hurejea kijijini.

Inadaiwa kuwa polisi waligundua kuwa simu ya padre huyo ilikuwa ikitumika kuwasiliana na wana mtandao wengine akiwamo baba mzazi wa Asiimwe, wakipanga njama za kutekeleza uhalifu huo.

Aidha, inaelezwa kuwa padre huyo ndiye aliyekuwa amemuunganisha baba Asiimwe na mganga wa jadi na pia ndiye alikuwa kiongozi katika kutafuta soko la viungo vya binti huyo.

Mwili ulivyopatikana

Wakati watu wengi wakiwa na imani kuwa juhudi za Polisi zinaweza kumuokoa mtoto huyo akiwa hai, jamii kuzunguka eneo hilo na nchi nzima ilifikwa na masikitiko makubwa asubuhi ya Juni 17, mwaka huu wakati mwili wa mtoto Asiimwe ulipopatikana ukiwa umetupwa chini ya kalavati katika barabara Ruhanga-Ntale kuelekea Kijiji cha Makongola ukitokea Barabara ya Kamachumu Muhutwe.

Eneo hilo ambalo lipo katika kijiji cha Luhanga ni takribani kilometa tatu kutoka nyumbani kwa mtoto Asiimwe kijiji cha Mbale.

Inaaminika kuwa mwili huo ulitupwa nyakati za usiku ukiwa umefungwa kwenye mfuko wa sandarusi.

Ulipofunguliwa ilibainika kuwa baadhi ya viungo vya binti huyo vilikuwa vimekatwa, ikiwa ni pamoja na ulimi, viganja vya mikono yake yote.

Inaendelea Uk. 10



Mkuu wa Jeshi la Polisi - Camillus Wambura.

Habari



Mabaki ya mwili wa mtoto Asiimwe ukipakiwa kwenye gari.

Hatua kwa hatua Asiimwe alivyotekwa, kuuawa

Inatoka Uk. 9

Baadhi ya watu waliokamatwa na Jeshi la Polisi walikuwa na mabaki ya mwili wa binadamu ambayo yanahisiwa kuwa ni viungo vya Asiimwe.

Viungo hivyo vimepelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uchunguzi.

Padre asimamishwa

Kukamatwa kwa padre huyo kulizua mjadala mizito mitandaoni kukiwa na taarifa zinazokinzana kuhusiana na mtumishi huyo wa kanisa.

Baadhi ya taarifa zilidai kuwa mtu huyo siyo padre kama inavyodaiwa, bali ni mtu anayefahamiana na paroko katika eneo hilo ambaye aliamua kumhifadhi kutokana na uraibu wake wa ulevi.

Wengine walidai kuwa kweli kijana huyo ni padre ambaye ametopea katika ulevi.

Mzizi wa fitna wa suala hilo ulikatwa Ijumaa iliyopita pale Kanisa Katoliki, Jimbo la Bukoba lilipotangaza kumsimamisha Padre Elipidius Rwegoshora, kutoa huduma za kichungaji kufuatia kuhusishwa kwake na tuhuma za utekaji na mauaji ya mtoto Asiimwe.

Askofu wa Jimbo Katoliki Bukoba, Jovitus Mwijage, alitangaza uamuzi huo kupitia gazeti la Kiongozi, linalotolewa na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), toleo lake la Juni 21 - 27, 2024.

Gazeti hilo lilimnukuu Askofu Mwijage aki-

kiri kuwa mtuhumiwa ni padri wa jimbo lake na amemsimamisha kutoa huduma zote za kichungaji mpaka hapo suala lake litakaposhughulikiwa na vyombo vya sheria.

“Tunahuzunishwa na taarifa ya mauaji ya Asiimwe, kwani sisi kama Kanisa Katoliki ni walinzi wa kwanza wa uhai wa wanadamu. Tunaiombea familia yake na kuiombea roho yake ipate pumziko la amani mbinguni.

“Hata hivyo, tumesikia taarifa ya watuhumiwa na mmojawapo akiwa ni Padri Rwegoshora. Ni kweli padri huyo ni wa jimbo Katoliki Bukoba na tumechukua uamuzi wa kumsimamisha kutoa huduma zote za kichungaji mpaka hapo suala lake litakaposhughulikiwa na vyombo vya sheria.

“Baada ya vyombo vya sheria kumaliza kazi yake, ndipo taratibu nyingine za kanisa zitafuata,” alisema Askofu Mwijage.

Wananchi Dar, Mwanza wazungumza

Baada ya kuwepo kwa taarifa za kifo cha Asiimwe na baadaye kuokotwa kwa mwili wa binti huyo ukiwa umenyofolewa ulimi na kukatwa viganja vya mkono, waandishi wa Pambazuko walioko Mwanza walizungumza na baadhi ya watu ambao wamelaani tukio hilo la kinyama na wengi kuhoji – “hivi kwanini mauaji haya yanarejea sasa?”

Kutoka Dar es Salaam, Mwanaidi Athuman, mkazi wa Tandika amelaani tukio hilo na kuitaka serikali kuongeza nguvu kulinda watu wake, hasa wale wenye ualbino, kwani wanapouawa ama kupotea, Tanzania inapata aibu na kuonekana watu wake wengi “bado wajinga na washamba.”

Baba wa Taifa na kuwepo mizengwe

Na Dkt. Benson BAGONZA

MIZENGWE na fitna havikuanza baada ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuondoka madarakani.

Hata wakati wake, wapo waliojaribu kuanzisha mizengwe na fitna za kisiasa. Tofauti ya wakati ule na huu wetu wa sasa, ni moja tu; wakati wa Baba wa Taifa, mizengwe na fitna ilianzishwa na wapambe na makanda bila kumhusisha.

Mwalimu Nyerere alipogundua, aliikemea na kuikomesha. Wakati fulani alimwajibisha kada na msaidizi wake kipenzi, Paul Sozigwa, baada ya kugundua kuwa anawalazimisha watu kuchangia harambee ya ujenzi wa kanisa fulani huko Dodoma, kwa kisingizio cha kumuunga mkono Baba wa Taifa.

Wakati wetu wa sasa, wapanga mizengwe na fitna, wanadiriki ama kuwahusisha wakuu wa mihimili au wanaanzisha mizengwe na fitna na hawawajibishwi.

Mizengwe na fitna hizo, vinawachonganisha wakuu wetu na wananchi au hata kuwachafua kuwa wakuu ndio wamewatuma hao wafanya mizengwe na fitna.

Imewapasa wakuu wetu kukemea mizengwe na fitna kwa namna ambayo haiachi mashaka kuwa wanahusika na mizengwe hiyo.

Na iwe kwamba - “mtu akiwatazama usoni ajue kuwa wanamaanisha wanachokikemea”. Hii ni kwa sababu baadhi ya mizengwe na fitna ina sura ya kijinai, mingine inavunja katiba, na mingine inapunguza viwango vya kimaadili.

Kibaya zaidi, baadhi ya mizengwe na fitna vinafanyika ndani vyombo vyenye utakatifu wa taifa letu.

Katika kukemea na kujitenga na mizengwe hiyo, Baba wa Taifa daima alizingatia mambo matano:

Kwamba Ikulu ni mahali patakatifu. Utakatifu wa Ikulu haukutokana na utakatifu wa Baba wa



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere

Taifa, bali msimamo wa wazi kuwa yeyote atumikaye Ofisi Kuu, aendaye Ikulu atatenda na kutekdewa haki, siyo pungufu ya haki.

Kwa muda mrefu na kwa nyakati tofauti wakati wa Mwalimu Nyerere, Mzee Timothy Apiyo na John Rupia walikuwa kama makuhani wa madhabahu ya Ikulu.

Chochote kinyonge na kisicho cha nuru, haki kuhusishwa na Ikulu. Waliofuata waliiga mfanohuu isipokuwa hawakuwa waangalifu katika uteuzi wa “makuhani.”

Kwamba chama tawala kilikuwa kisafi kuliko serikali na Mwalimu Nyerere alilalamika kuwa matendo ya serikali yalikuwa yanakichafua chama.

Inaendelea Uk. 12

Tafakuri

Baba wa Taifa na kuwepo mizengwe

Inatoka Uk. 11

Msimamo wa kutenganisha chama na serikali ulilenga kukifanya chama kuwa mfano na kielelezo kwa serikali. Chuo cha Kivukoni, JKT na madarasa ya itikadi, vililenga kutatua kasoro hii.

Kwamba pamoja na uwepo wa washauri wa rais, Mwalimu Nyerere alipata ushauri wake wa msingi kutoka kwa watu wa kawaida.

Aliwauliza wapishi, wafagiaji, wakulima sham-bani, wacheza bao, madereva, wanafunzi na waumini wa kawaida kanisani Butiama ikiwa waliuelewa Ujamaa na Azimio la Arusha.

Nyakati fulani alimwuliza hata mama yake mzazi. Hekima ya kweli imesheheni katika watu wa kawaida na ndio maana Mungu ameumba wengi mno.


Ni muhimu sana kwa wakuu wetu kujilinda na chachu ya watu kutoka 'jalalani' hata kama elimu yao ni muhimu pia.

Kwamba Mwalimu Nyerere aliwasikiliza washauri wake rasmi kwa kila sekta bila yeye kuwashauri. Wakati mwingine alifanya kama utani na kukaa na kuwaita waje kumshauri na aliwasikiliza na kuwauliza maswali magumu baada ya kuwasikiliza.

Matokeo yake, washauri wake walilazimika kuandika ripoti zao na kumpa mapema azisome. Alizisoma na kuzichafua kwa kalamu ili kuwonyesha alipokuwa na mashaka.

Kwamba, kwa sababu za kihistoria, Mwalimu Nyerere aliona maadui wengi nje kuliko ndani. Maadui wa nje aliona ni mabeberu na mabepari. Maadui wa ndani aliona ni viongozi na vibaraka.

Alitumia muda mwingi na timu ya mambo ya nje kutafakari matishio ya nje kuliko ya ndani. Hii ilimsaidia kuwatania Watanzania aliowaita



Paul Sozigwa

“Waswahili” ambao aliona wanasumbuliwa zaidi na ushamba, ujinga, maradhi na umaskini.

Kundi la pili la maadui wa taifa aliona ni viongozi vibaraka kuliko “Waswahili.”

Sikumbuki wakati wowote Mwalimu Nyerere alipoona wananchi ni tatizo na kuwatungia sheria ya kuwadhibiti.

Aliwakomalia viongozi ambao daima aliona wanataka kutumia ujinga wa wananchi ili kuwanyonya na kuwakandamiza.

Kutokana na misimamo hii ya Mwalimu Nyerere, haya yalitokea; kuna watu walikufa wakaandika urithi wa mali zao kwa serikali au kwa chama tawala. Serikali na chama vilikuwa na hadhi sawa na dini.

Pia kuna watu waliwekesha mali zao serikalini na kwenye chama. Watu walilaza magari yao kwenye viwanja na ofisi za Tanu na baadaye CCM, kuliko kuyalaza kanisani au msikitini.

Lakini zaidi sana, watu walipeleka mashauri yao Tanu/CCM kuliko kuyapeleka mahakamani. Halafu kadi ya Tanu/CCM ilikuwa na uzito kuliko passport au shahada ya chuo kikuu.

Ni wakati wa Mwalimu Nyerere, tulifuta ujinga kitaifa tukiwa na chuo kikuu kimoja, lakini hivi sasa tuna vyuo vikuu zaidi ya 50 ila tuna wajinga wengi!

Ukiona wazee kama mimi tuna kumbukumbu nyingi kuliko ndoto za kesho, ujue kuwa kuna jambo lisilo sawa mahali fulani.

Kutukanwa ni halali yangu maana nimepitwa na wakati. Nikiitwa mzee mzima ovyo nitakuwa nimependelewa.

What went wrong? Nini kilienda mrama?


Mwandishi wa tafakuri hii ni Askofu wa Kanisa la Kilutheri la Kiinjili Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji wa makala Pambazuko.

Mezani kwa Chahali



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mnawaza kufungia X, bado kuna TikTok!



WAKATI shinikizo likiendelea nchini Tanzania kuitaka serikali ifungie mtandao wa kijamii wa X (zamani Twitter) kwa madai kuwa unahamasisha maudhui yaliyo kinyume na maadili ya Kitanzania, wiki hii imedhihirika huko Kenya kuwa mtandao mwingine wa kijamii wa TikTok “ni hatari zaidi” kuliko huo unaopigiwa chapuo ufungwe.

Japo ni kweli kwamba mitandao ya kijamii inaweza kuwa “hatari”, neno “hatari zaidi” hapo juu limetumika makusudi, kwa muktadha wa kudaka mwanngwi wa wale wote wanaotaka udhibiti dhidi ya mitandao hiyo ya kijamii.

Kwa siku kadhaa wiki iliyopita, vijana mbalimbali nchini Kenya wameshiriki kwenye maandamano makubwa kupinga muswada wa fedha uliowasilishwa kwenye bunge la nchi hiyo ya Afrika Mashariki.

Vijana hao wanafahamika zaidi kwa jina la Generation Z (Kizazi Z) kwa kifupi Gen-Z.

Kuna vizazi kadhaa ambavyo kwa kiasi kikubwa vinaambatana na matukio muhimu duniani. Hata hivyo, vizazi hivi vinaweza kutoleta maana sana kwa nchi zisizo za ‘Kimagharibi’ kwa sababu matukio makuu yanahusu nchi za Magharibi.

Kizazi Kilichopotea (Lost Generation) - 1883-1900

Kizazi cha Wakuu Sana (Greatest Generation) - 1901-1927

Kizazi cha Kimya (Silent Generation) - 1928-1945

Baby Boomers - 1946-1964

Kizazi X (Generation X) - 1965-1980

Kizazi cha Milenia (Millennials) - 1981-1996

Kizazi Z (Generation Z) - 1997-2012

Kizazi Kipya (Generation Alpha) - 2013-hadi sasa.

Kwanini TikTok imekuwa na ufanisi sana kwa vijana hao kuhamasishana kushiriki maandamano yanayoendelea?

Moja ya sababu kubwa ni ukweli kwamba TikTok ni mtandao wa kijamii wa video zaidi na picha kidogo, ilhali Twitter ni maandishi zaidi.

Sababu nyingine ya msingi ni kwamba TikTok ina watumiaji wengi zaidi kuliko X/Twitter. Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni,

TikTok ina takriban watumiaji bilioni moja kwa mwezi ilhali X/Twitter ina takriban watumiaji milioni 600 kwa mwezi.

Kadhalika, tofauti na X/Twitter ambayo kimsingi ni mtandao wa kijamii uliojikita zaidi kwenye habari, TikTok ni ya burudani zaidi huku video nyingi zikionyesha watumiaji mbalimbali wakicheza muziki ama kushiriki burudani kadhaa kwa lengo hasa la kuondoa msongo wa mawazo.

Tukiweka kando ufanisi wa TikTok unavyowawezesha vijana wa Kenya kushiriki maandamano yanayoendelea, maandamano hayo yanapaswa kufikisha ujumbe kwa watawala wetu kwamba – ingawa mazingira ya Kenya na Tanzania ni tofauti, nguvu ya vijana inaweza kusababisha mabadiliko makubwa kwenye jamii.

Lakini, mabadiliko hayo hayapaswi kuwa dhidi ya watawala, bali endapo vijana watawezesha ipasavyo, wanaweza kuleta mabadiliko yenye manufaa kwa taifa zima, huku jamii ikifaidika na mtandao huo.

https://instagram.com/evarist_chahali



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Brela imeonyesha njia, wengine wafuate



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Brela - Godfrey Nyaisa.

NI kipindi kirefu sasa tumekuwa tukisikia mvumo wa viongozi wa serikali pamoja na mashirika ya umma Tanzania kuwataka waandishi wa habari kuandika juu ya kazi na mafanikio ya taasisi hizo, badala ya kujikita kuandika habari za ukosoaji pekee.

Hata mimi na wewe pia tungetamani waandishi wa habari kila kukicha wawe wanaandika namna mashirika, kampuni na taasisi zetu zina-
vyotekeleza majukumu yake kitaifa.

Wengi tungetamani wafanye hivyo ili wananchi waelewe kwa kina namna huduma zina-
vyotolewa katika taasisi zetu zote.

Hata hivyo, kinachostaajabisha licha ya matamano haya mazuri ya viongozi wengi wa taasisi za serikali pamoja na mashirika ya umma, kuwataka taarifa zao zisomeke, zisikike na kuonekana kwenye vyombo vya habari, hayakamiliki kutokana na kuwa na matobo mahala.

Tena matobo makubwa yasiyohitaji darubini kuyaona ambayo Wizara ya Viwanda na Biashara, mithili ya mtu aliyetoka usingizini, imeyao-
na na kuamua kuchukua hatua haraka kuyaziba kabla mambo hayajaharibika!

Ni kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela) imejifunga kibwewe na kuamua kuwatoa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam na kuwapeleka Morogoro kwa lengo la kuwanoa kuhusu namna wanavyoweza kuwa mahiri katika kuandika habari zinazohusu shughuli za Brela.

Mafunzo hayo maalumu kwa waandishi wa habari yalianza rasmi Juni 18 hadi 21, 2024 yalifunguliwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Abdallah.

Dkt. Abdallah, alisema dhamira kuu ya mafunzo hayo ya siku nne ni kuwaelimisha waandishi wa habari kuhusu taratibu za usajili wa biashara na leseni za kampuni.

Ileweke kuwa elimu kwa wanahabari ni muhimu sana kwani wao ndiyo walimu wanaosambaza wanayofahamu kwa umma. Ndiyo maana inasemwa – kumuelimisha mwanahabari, ni kuelimisha jamii.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba waandishi wa habari ndio daraja kati ya taasisi kama Brela na umma. Kwa kutoa taarifa sahihi na za kina kuhusu taratibu za usajili wa biashara na

leseni, wanahabari wanaweza kusaidia sana kukuza uelewa na uwazi kwa wananchi.

Ikiwa mwanahabari ataelewa kwa undani namna taasisi, shirika na kampuni zinavyofanya kazi, ni rahisi zaidi kupeleka elimu hiyo kwa wananchi ili watambue nini hasa kinafanyika huko.

Kutokana na Brela kuchukua hatua hiyo, ni wakati muafaka sasa kwa taasisi nyingine za serikali na hata binafsi, kufuata nyayo za Brela kwa kuwapa elimu waandishi wa habari kuhusu utendaji wao wa kazi ili nao “wawalishe” wananchi.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546/ email; mtagaluka@gmail.com

Habari

Polisi ndani ya tope la kashfa

Inatoka Uk. 4

“Askari polisi walisisitiza kwamba Baraka amedhaminiwa, lakini nilipowabana kwa maswali zaidi kuhusu huyo aliyemdhamini, walikataa kunipa ushirikiano...”

“Kwa hiyo, niliwaomba askari wakigawe kile chakula kwa mahabusu wengine, kwani siwezi kurudi nacho nyumbani. Baada ya kukipokea, nikaondoka...”

“Jana hiyohiyo (Juni 12), saa 10 jioni, nilipata taarifa, kwamba kuna maiti imeokotwa majini ikiwa inaelea na nilipokwenda kuiona, nilikuta ni mwili wa ndugu yangu Baraka ambaye polisi waliniambia alikuwa amedhaminiwa...”

“Kibaya zaidi ni kwamba, ule mwili ulikuwa umefungwa kamba na inaonekana alitupwa mapema, ndiyo maana mwili ulikuwa umevimba...”

“Wengi tunaamini alifungwa jiwe kabla ya kutupwa, maana kama isingekuwa hivyo, lazima angeonwa tu na watu, maana hiyo sehemu kuna watu wengi wanafanya shughuli zao...”

“Kilichowakera wananchi ni kwamba, mwili huo ulipoonekana majini, askari polisi walitaka kuuzika haraka haraka, lakini wananchi wakagoma kwa sababu hawakuridhishwa na mazingira ya kifo hicho,” anasimulia Ibrahimu.

Kutokana na hali hiyo, Ibrahimu alisema askari polisi walipoona wananchi hawaridhishwi na kifo hicho na hivyo kutaka kuhatarisha amani kisiwani hapo, walilazimika kurusha mabomu ya machozi ili kuwatawanya wananchi waliokuwa na hasira.

Pamoja na hayo, alisema askari polisi wa kituo hicho waliomba msaada wa askari wengine waliowasili kutoka Kituo Kikuu cha Polisi, Wilaya ya Muleba wakiwa na silaha ili kutawanya umati ulioanza kuwa mkubwa kushuhudia sakata hilo.

Hospitali wazungumza

Gazeti la Pambazuko lilifika hospitali ulioko pelekwa mwili kwa ajili ya uchunguzi, kama walivyodai Polisi, lakini imebainika kuwa hadi jana jioni, hakuna uchunguzi wowote wa kitabu uliofanywa kuchunguza chanzo cha kifo cha Baraka.

Akikataa kutaja jina lake gazetini, ofisa mmoja wa Hospitali ya Mkoa wa Kagera, alisema wao walipokea mwili na kuuhifadhi chumba cha maiti, bila kupewa majukumu mengine.

“Sisi tuliletewa mwili kuuhifadhi, hayo mengine ya uchunguzi, mimi sijui, labda wenzangu. Waulize wao,” alisema ofisa huyo.

Inaendelea Uk. 22



RPC Kagera- Chatanda

Habari

Na Mwandishi WETU

WAFANYABIASHARA wanaoagiza bidhaa kutoa nje ya Tanzania, wamepewa siri ya kutengeneza faida kubwa kwenye shughuli zao; kuwa ni kutumia meli kubwa kuleta mizigo yao.

Meneja Mizigo Mchanganyiko wa Bandari ya Dar es Salaam, Abed Gallus amewaasa wafanyabiashara kuwa mafanikio ya kupata faida kubwa ni kuagiza kwa wingi bidhaa ambazo zinakuja kwa pamoja.

Abed ametoa ushauri huo juzi; Jumamosi – Juni 22, jijini Dar es Salaam wakati akishuhudiwa kutia nanga kwa meli kubwa zaidi kuwahi kufanya hivyo katika bandari hiyo muhimu kwa uchumi na ustawi wa Tanzania.

Meli hiyo - MSC ADU 5, iliyokuwa imebeba makasha 4000, ilitia nanga katika kina kili-chofanyiwa maboresho hivi karibuni, cha mita 12.5, ambacho kimefanikisha kufika kwa chombo chenye ukubwa zaidi.

“Miongoni mwa fursa kubwa kwa wafanyabiashara wetu, ni kutumia bandari yetu zaidi kwani sasa ina uwezo wa kupokea meli kubwa zinazobeba makasha mengi kwa wakati mmoja...

“Kutumia meli kubwa za mizigo kubeba bidhaa na kuleta Tanzania, kunapunguza gharama za ku-safirisha, ambapo zinaleta unafuu kwa wafanyabiashara na wasafirishaji wa mizigo sambamba na kuchochea ushindani wa bandari zilizopo ukanda wa Afrika Mashariki na Kati,” ameingiza Abed.

Kuwasili kwa meli hiyo katika Bandari ya Dar es Salaam kunaweka rekodi mpya ya kupokea meli kubwa ya mizigo yenye urefu wa mita 294.1, tofauti na meli ambazo zimewahi kutia nanga

TPA yawapa siri wafanyabiashara kufanikiwa


nchini. Meli kubwa ya mwisho kupokelewa ilikuwa na urefu wa mita 267.

“Hii ni historia kwetu kwani hapo awali tulikuwa tunapokea meli zenye urefu wa mita 267, lakini kuanzia leo tunaweza kupokea meli zenye ukubwa wa mita 305, haya ni mafanikio makubwa kwetu,” ameingiza Abed.

Abed alisema Bandari ya Dar es Salaam ni miongoni mwa bandari sita ambazo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inazisimamia na kwa kuliona hilo imeendelea kuboresha bandari nyingine ili kutoa msaada kwa Bandari ya Dar es Salaam ambayo zaidi ya asilimia 90 ya mizigo inapita katika bandari hiyo.

“Tumendelea kuboresha miundombinu ya bandari zetu zingine ikiwemo pamoja na bandari ya Mtwara na Tanga ambapo tayari tumeshanunua vifaa vya upakuaji mizigo kwani hapo awali Bandari ya Tanga, meli zilikuwa zinafungwa nje ya gati, lakini sasa hivi meli zinaingia kwenye gati. Maboresho haya yote ni juhudi za mamlaka kuhakikisha bandari hizo zinatoa msaada kwa Bandari ya Dar es Salaam,” amesema Abed.

Katika kufanya kazi kiushindani sambamba na kujiimarisha kibiashara, TPA imeingia mikataba ya kiuendesha katika baadhi ya gati zake kwa Bandari ya Dar es Salaam, ili kuongeza ufanisi.



Meli kubwa ya mizigo ya MSC ADU-V yenye urefu wa mita 294.1 na uwezo wa kubeba makontena 4000 ikiwasili katika Bandari ya Dar es Salaam jana. (Picha na Mpigapicha Wetu).



Mbunge wa Viti-Maalum (CCM), Neema Lugangira, akimfariji mama mzazi wa mtoto Asimwe (kulia), aliye-fariki hivi karibuni kwa kukatwa viungo vyake kiha kutupwa barabarani mkoani Kagera. (Na Mpigapicha Wetu).

Mbunge, UWT waandamana kumlilia Aimwe

**Na Mwandishi WETU,
Muleba**

KIFO cha kikatili cha mtoto mwenye ualibino, Aiimwe Novath kimemuibua Mbunge wa Viti-Maalum, Neema Lugangira, aliye-itiha maandamano kulaani mauaji hayo.

Maandamano hayo yaliyofanyika Mjini Bukoba Jumatano iliyopita – Juni 19, na baadaye waandamanaji, wengi wakiwa wanachama wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani humo, walikwenda kuhani miba nyumbani kwa binti huyo na kufika eneo alikozikwa.

Akizungumza na waandamaji na waombolezaji wengine katika kijiji cha Bulamula, Kata ya Kamachumu, Muleba mkoani Kagera, Mbunge

Lugangira aliwailiha alamu za pole kutoka kwa Rai amia uluhu Haan, na kuwahakikihia kuwa erikali, kupitia vyombo vya ualama, inaendelea kuchunguza na kwamba “wahuika wote, watakatwa na kuchukuliwa hatua za kiheria.”

Mwili wa Aiimwe ulikutwa umetupwa kwenye karavati ukiwa umekatwa na kunyofolewa baadhi ya viungo vyake vya mwili; mikono na ulimi, katika Kijiji cha Marere, Kata ya Ruhanga, Wilaya ya Muleba –iku 19 baada ya kutekwa kwake.

Binti huyo wa miaka miwili na nuu, alitekwa na watu waiofahamika nyumbani kwao Mei 3 mwaka huu, karibu majira ya aa mbili ukiu baada ya watu wawili kuomba maada wa chumvi kwa mama yake, kiha kumkaba – na kumwacha akiwa amezirai, na kuteka mtoto na kutoweka naye kuikojulikana.

Mwana Diaspora

Na Jerry MURO



Je, Tanzania inakopa kujikwamua, au?

NAREJEA ziara rasmi ya kikazi ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyofanya Korea Kusini na baadaye kuungana na baadhi ya viongozi wa Afrika waliohudhuria mkutano mahsusi wa pamoja nchini humo.

Mengi yamesemwa, lakini hapa nachambua mambo mawili makubwa kwa lugha nyepesi ambayo wengi wanaweza kuelewa.

Mosi, kusainiwa kwa mkataba wa miaka mitano wa makubaliano kati ya Tanzania na Korea Kusini, ambao utaiwezesha nchi yetu kupata mkopo wa masharti nafuu wa kiasi cha dola za Marekani bilioni 2.5 (zaidi ya Shilingi trilioni 6).

Mkopo huo ambao unatolewa na Taasisi ya EDCF ya Korea Kusini, utawekwa kwenye Hazina ya Tanzani kwa kipindi cha miaka mitano na nchi yetu itatakiwa kuanza kurejesha baada ya kipindi cha miaka 25.

Hii maana yake ni kwamba katika kurejesha Tanzania itatakiwa kurejesha ndani ya kipindi cha miaka 40, kwa formula ya 5-25-40.

Imeelezwa kwamba fedha hizo ni kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu, ambapo sasa serikali itakuwa na wajibu wa kuwaeleza wananchi ni miundombinu ipi, iko wapi na kiasi gani kitatumika kwa nini?

Lakini pia, serikali lazima ieleze matumizi ya fedha hizo yana tija gani kwa mwananchi anayekwenda kuulipa mkopo huu?

Katika ukopaji huu, wako baadhi ya watu wanauliza Korea Kusini ananufaika nini na Tanzania? Jibu ni kwamba, bado Tanzania imekuwa soko kubwa la Korea Kusini ambapo wao ndiyo wanatutengenezea treni ya umeme na mabehewa yake.

Kwamba Reli ya SGR kuanzia Lot 1 hadi 5 na vitu vingine, ikiwemo vifaa vya kielektroniki; mfano simu na mitambo ya ujenzi kutaja vichache, vinatoka Korea Kusini.

Tofauti ya mkopo huu na ile mingine ya kibiashara, huu una riba

ndogo tofauti na ile mingine inayotolewa kwa masjharti magumu.

Pili, Jambo ambalo natamani wenzangu Watanzania kulitazama kwa umakini, ni kusainiwa kwa tamko la pamoja la kuanzishwaji kwa majadiliano ya ushirikiano wa kibiashara na uchumi, ambayo yatachochea kwa kiasi kikubwa kuanza kuwepo kwa mafanikio makubwa ya kufanya biashara na Korea Kusini katika maeneo mengi yakiwamo ya uwekezaji, viwanda na usafirishaji.

Baada ya makubaliano hayo, sasa Korea Kusini inatarajiwa kupanua wigo wa ushirikiano wa kufanya biashara kwa lengo la washirika wote kupata zaidi na kunufaisha nchi zetu.

Ni kutokana na ushirikiano huo, Watanzania tunatakiwa kujipanga kimikakati ili kuchangamkia fursa zinazotoka Korea Kusini.

Mipango ya kimkakati na maandalizi yanayotokana na makubaliano hayo ni muhimu sana kuwekwa mezani na wananchi kuzitambua fursa zilizopo ili “wafanye kweli.”

Nayo serikali kupitia wataalamu wake wapange vyema hatua za kufikia mafanikio ya ushirikiano huo na taifa kubwa na kuweka agenda bobezi zinazoendana na mipango endelevu ya taifa ya muda mfupi na mrefu huku tikiwa na taswira ya kutanguliza maslahi ya wananchi wetu.

Nimefurahi kuona katika ziara hii pande zote katika muungano zimevuna kupitia hati mbili za makubaliano katika hatua ya awali; huku Zanzibar wakiwa wamepata mengi kupitia Uchumi wa Blue ambako tekhnojia ya utafiti wa mazoa ya majini na rasilimali zake, sasa utakua maradufu.

Mwandishi wa safu hii ni mwanafunzi wa shahada ya zzamili (Masters Degree in Strategic Governance) katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim, Kurasini, Dar es Salaam.



Rais Samia Suluhu Hassan



Mamilioni ya mabinti wachanjwa kuzuia kansa ya shingo ya kizazi

NIGERIA imetoa chanjo dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wasichana milioni saba nchini humo, ugonjwa unaowaathiri zaidi wasichana wadogo.

Kampeni hiyo ya wiki mbili ni hatua kubwa katika kuwalinda wasichana wadogo na wanawake dhidi ya ugonjwa huo wenye kutishia uhai wa binadamu. Saratani pia hujulikana kwa jina la kansa, ikiwa ni matokeo ya kutoholewa kutoka Kiingereza; cancer.

Kampeni hiyo ya kuchanja, inasimamiwa na serikali, chini ya mpango wa shirika la kimataifa linalohusiana na masuala ya afya la Gavi, kwa ushirikiano na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef) na Shirika la Afya Duniani (WHO).

“Ni mafanikio makubwa katika afya ya wasichana nchini Nigeria. Katika wiki mbili tu, wasi-

chana milioni saba wamechanjwa dhidi ya virusi vya HPV,” amesema Sania Nishtar, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Gavi.

HPV huambukizwa kwa njia ya kujamiiana na huweza kusababisha saratani ya shingo ya kizazi.

Oktoba mwaka 2023, Nigeria ilitambulisha awamu ya kwanza ya chanjo dhidi ya virusi vina-vyosababisha magonjwa ya zinaa kama hatua ya kukabiliana na maradhi hayo, ambayo yanashika nafasi ya pili kati ya kansa zote zinazowakumbuka wanawake duniani.

Waziri wa Afya wa Nigeria, Muhammad Ali Pate amesema kuwa chanjo hiyo inawalenga wasichana wenye umri kati ya miaka tisa hadi 14 na kwamba itakuwa endelevu ili kuhakikisha hatari ya ugonjwa huo inapungua zaidi.

Chanzo: TRT - Africa

Mtoto wa Mvuvi

Na Maregesi PAUL



Wananchi Nafuba waungwe mkono

HIVI karibuni, nilikuwa wilayani Bunda, Mkoa wa Mara, ambapo nilifika kijijini kwetu katika Kata ya Nansimo ambayo ni moja ya kata zinazounda Jimbo la Uchaguzi la Mwibara.

Niliwatembelea ndugu na marafiki zangu katika vijiji mbalimbali kikiwamo Kisiwa cha Nafuba kilichoko katika Ziwa Victoria ambacho pia ni sehemu ya vijiji vinavyounda Kata ya Nansimo.

Nilitembelea Nafuba, kwa sababu niliambiwa wananchi wa kijiji hicho, wanajitolea kusomba na kupanga mawe ili wapate barabara ya kudumu kisiwani kwao kwa kuwa moja ya changamoto zinazowakabili ni ukosefu wa barabara za kudumu.

Nilipofika Nafuba kupitia Kitongoji cha Kirongo, nilishuhudia jinsi wananchi hao walivyohamasishana na kushirikiana kufanikisha ujenzi wa barabara hiyo kupitia mikono yao.

Nilifika eneo la Togosi, kisha nikaelekea Ikolokolo ambako ndiko hitimisho la ujenzi wa barabara hiyo inayoelezwa kuwa na urefu wa zaidi ya kilomita mbili.

Hakika, kwa kuwa wananchi wa Nafuba wameshikamana, wanahitaji msaada kukamilisha mradi huo wanaotekeleza kwa nguvu zao bila kujali hali zao za uchumi.

Kwa kuwa jukumu langu lilikuwa ni kutaka kuufikishia umma taarifa za kinachoendelea kisiwani humo, nilizungumza na watu mbalimbali ili kuona kama serikali na baadhi ya viongozi wa kisiasa, wameshaunga mkono jitihada zao.

Kwa mujibu wa baadhi ya wananchi hao, wakati huo walikuwa hawajaungwa mkono na serikali, ingawa wadau mbalimbali wa maendeleo walikuwa wameshawafikishia mis-

aada kadhaa.

Pamoja na hayo, bado serikali na wadau wote wa maendeleo wakiwamo baadhi ya wanasiasa ambao hawajajitokeza kutoa misaada, hawajachelewa kuwafikia na kuwaunga mkono kwa sababu muda bado upo na mahitaji bado yapo.

Ni wakati sasa viongozi wa wilaya hiyo, taasisi za umma na binafsi, kufanya kila linaloezekana kuwaunga mkono kwa fedha, vifaa na hata utaalamu wa kuwahakikishia wanapata barabara bora na inayoweza kudumu kwa muda mrefu.

Na pia natoa mwito kwa viongozi wa mkoa huo kuacha kujifungia ofisini kwao Musoma Mjini, waamke, wajaze mafuta magari yao, wangoze misafara kuelekea Nafuba ili kuchochea hamasa ya maendeleo inayofanywa na wananchi hao.

Viongozi wa kisiasa nao wasibaki nyuma, ni wakati wao kukitembelea kisiwa hicho ili kuwashika mkono wananchi wa Nafuba.

Wananchi wa Nafuba hawatakiwi kuachwa kama yatima, bali kuungwa mkono ili nao wao one kuwa sehemu ya wananchi wanaoiunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kinachofanywa na wananchi wa Nafuba hakipaswi kufumbiwa macho na naamini kama wananchi hao wataungwa mkono kwa namna yoyote ile, siku zijazo wanaweza kufanya mambo makubwa ya maendeleo tofauti na inavyofikiriwa kuwa kila mafanikio ya sehemu, lazima kuwepo mkono wa serikali.





*Mwanasayansi
mtafiti akiwaa-
chia mbu mad-
ume walioahasi-
wa katika kisiwa
cha Captiva huko
Florida nchini
Marekani.*

Malaria yapigwa vita kwa kuwahasi mbu

Na Mwandishi WETU

TEKNOLOJIA inakua kwa kasi sana. Hivi sasa wanasayansi wamebaini utalaamu wa kuhasi mbu kama njia mbadala ya kupambana na magonjwa ya kuambukizwa, ikiwamo malaria.

Katika njia hiyo, wanasayansi wanawalenga mbu ambao wamekuwa sugu kwa dawa zinazotumika kuwaangamiza na kuwahasi. Hiyo imeweze sha kuua kabisa kizazi chao baada ya muda mfupi.

Utaalamu huo, ambao bado unaendelea kufanywa utafiti, umetangazwa na wanasayansi kutoka Fort Myers huko Florida, Marekani. Teknolojia hiyo mpya inalenga kuongeza kasi ya kupambana na malaria hasa katika nchi za kitropiki.

Mradi huo wa majaribio unafanyika kwa ushirikiano wa ufadhili na watalaamu kutoka Wakala wa Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na unalenga kuzuia mbu kuzaliana kwa wingi, ikiwalenga mbu wa jamii ya *Aedes Aegypti*, ambao wanapatikana kwa wingi huko Florida.

Jamii hiyo ya mbu ni wagumu kuwadhibiti kwa kutumia njia za kawaida kwa sababu wanazaliana katika maeneo ambayo ni vigumu kuwabaini lava wao na kuwaangamiza.

Aidha, mbu hawa wameshaanza kujenga usugu wa kemikali zinazotumika kuangamiza mbu. Kituo cha kudhibiti mbu cha Kaunti ya Wuilaya ya Lee (LCMD), kilichopo kusini mashariki mwa Florida, kimekuwa kikifanya utafiti wa kuwadhibi-

ti mbu hao ili wasilete madhara makubwa kwa jamii tangu mwaka 1958.

Lakini ongezeko la idadi ya watu mijini na uwezo wa mbu hao kujikinga dhidi ya dawa zinazotumika kuwaangamiza, kumesababisha iwe vigumu kuwadhibiti katika miaka ya hivi karibuni.

Hilo limesababisha LCMD kutafuta njia mbadala za kuwakabili mbu hao.

Moja ya njia mpya zinazofanyiwa utafiti ni kuwahasi mbu dume wa jamii hiyo (SIT) kama njia ya kudhibiti kuzalina kwao.

SIT imeonekana kuwa ni njia nzuri kwa sababu pamoja na faida nyingine, lakini pia haiharibu mazingira kama matumizi ya kemikali.

Mbu dume wa jamii hiyo huasiwa kwa kutumia njia ya mionzi kabla hawajaachiwa kwenda kujamiiana na majike.

Lakini, kwa sababu wamehasiwa mbu hao hawawezi kuwazalisha majike, hivyo kufanya kizazi chao kupungua taratibu na hatimaye kutoweka kabisa.

Pamoja na kusambaza malaria, mbu janii ya *Aedes Aegypti* pia wanasambaza magonjwa mengine hatari kama vile chikungunya, homa ya dengue, homa ya manjano, na Zika, na kuwafanya kuwa hatari zaidi kwa jamii za nchi za kitropiki ambako wanastawi kwa wingi.

Juhudi hizi za kuhasi mbu inaaminika zitachangia kufikia lengo la tatu la Malengo Endelevu ya Milenia la kuwa na jamii yenye afya bora.

Majaribio ya kuwahasi mbu yalianza 2020 ambapo mbu wengi madume walifugwa na kuhasiwa kabla hawajachiwa kujamiiana na mbu majike.

Habari

Polisi ndani ya tope la kashfa

Inatoka Uk. 15

Kiongozi, Polisi wazungumza

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kishamba kisiwani hapo, Kanywani Max, alipozungumza na Pambazuko kwa njia ya simu, alithibitisha kuwapo kwa tukio.

“Ni kweli, kuna mvuvi mmoja alikamatwa kwa kosa la uzembe na uzururaji majira ya usiku kisha akashikiliwa katika kituo cha polisi hapa Goziba. Baadaye, mwili wake ulikutwa majini ukiwa unaelea na hadi sasa chanzo cha kifo hicho hatujakifahamu ingawa mwili wa marehemu umepelekwa Hospitali ya Mkoa wa Kagera kwa ajili ya uchunguzi zaidi,” alisema Max.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Kagera, Blasius Chatanda, alipopigiwa simu ili kuzungumzia tukio hilo, simu yake ilipokewa na mmoja wa askari polisi ambaye alieleza kuwa ofisini kwake ambaye aligoma kuzungumzia tukio hilo kwa kile alichoeleza kuwa hana mamlaka hayo.

“Afande RPC hayuko ofisini, yuko nje ya ofisi kuna tukio limetokea analifuatilia. Kwa hiyo, mimi siwezi kusema chochote, subiri kama dakika thelathini hivi nitakuunganisha naye,” alisema askari huyo.

Hata hivyo, baada ya nusu saa kupitia, simu hiyo ilipopigwa haikupokelewa tena hadi tulipokwenda mtamboni.

Msemaji wa Jeshi la Polisi Tanzania, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, David Misime, wiki iliyopita alipopigiwa simu mara kadhaa, hakupokea simu yake na hata alipotumiwa ujumbe mfupi wa maneno kuhusiana na tukio hilo, hakuujibu.

Hata hivyo, Juni 18, Misime alikutana na mwandishi wa gazeti hili na kumweleza kuwa tukio hilo tayari limetolewa ufafanuzi

na Jeshi la Polisi.

Mwandishi alipouliza taarifa hiyo imetolewa lini, Misime aliahidi kumtumia mwandishi wetu taarifa hiyo katika simu yake kwa ushahidi zaidi.

“Hiyo taarifa ya hilo tukio, imeshatolewa tayari, hebu nipe namba yako nikutumie hiyo taarifa,” alisema Misime.

Pamoja na mwandishi wetu kumpa Misime namba yake ya simu ya mkononi, taarifa hiyo hakutumiwa na alipomkumbusha kwa ujumbe mfupi wa maneno, hakujibiwa hadi jana saa 6:27 usiku wakati gazeti linaanza kusambazwa.

Mbunge azungumza

Tukio la kifo hicho cha Baraka lilizungumzwa pia bungeni, Dodoma na Mbunge wa Muleba Kaskazini, Charles Mwijage, ambaye aliitaka serikali kupitia Jeshi la Polisi, kufanya uchunguzi wa tukio hilo kwa kina ili haki itendeke.

Wakati huohuo, taarifa zilizopatikana baada ya mwili wa marehemu Baraka kuondolewa kisiwani hapo, zinasema askari polisi kwa kushirikiana na viongozi wa Kisiwa cha Goziba, walikuwa wakihaha kumshawishi Ibrahim ili akashiriki mazishi ya ndugu yake mjini Bukoba, ambaye hata hivyo alikataa.

Kwa mujibu wa taarifa hizo, Ibrahim alikataa kwa kile kilichoelezwa kwamba baba wa marehemu ambaye anaishi mkoani Kigoma, amemzuia asishiriki mazishi hayo kwa “namna yoyote ile” na asiuguse mwili wa kijana wake.

“Askari polisi na baadhi ya viongozi wa kisiwa hiki, walikuwa wanamshawishi Ibrahim akashiriki mazishi ya ndugu yake, lakini Ibrahim aliwakatalia kwa sababu amezuiwa na baba wa marehemu, ambaye pia hataki kufika Muleba kwa mazishi kwa kuwa anaamini Jeshi la Polisi kuhusika na kifo cha utata cha kijana wake,” alisema Ibrahim.

Hadi jana, mwili wa Baraka haukuwa umezikwa na taarifa zinadai hakuna dalili za kuuhi-fadhi kaburini. Umehifadhiwa chumba cha maiti hospitalini.



Mkuu wa Mkoa wa Kagera - Fatma Mwassa.

Uchambuzi



Rais Samia Suluhu Hassan akiteta jambo na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye kabla ya kufungua Kongamano la Pili la Maendeleo ya Sekta ya Habari jijini Dar es Salaam Juni 18, 2024. (Picha na Ikulu).

Nondo za Samia kwa vyombo vya habari

Na Maregesi PAUL

KAZI iliyobaki kwa vyombo vya habari sasa ni kujiamini, kujitutumua na kuacha woga, kwani mkuu wa nchi, Rais Samia Suluhu Hassan, amerejea tena kauli yake kuwa “haamini kuvibana vyombo vya habari.”

Mbali na kuirejea kauli hiyo, Rais Samia pia amevihimiza vyombo hivyo kufanya kazi kwa bidii na weledi kwa kuchambua, kukosoa, kushauri serikali ili Tanzania na watu wake, isonge mbele.

Rais aliyarejea hayo wiki iliyopita alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam wakati wa kongamano la kitaifa la maendeleo ya sekta ya habari nchini.

Katika hotuba yake ya ufunguzi wa kongamano hilo lililowaleta pamoja zaidi ya wadau 1,200 wa sekta ya habari, Rais Samia aliweka bayana “nondo tano” kwa wadau na aliazna kwa kuonyesha jinsi alivyo tayari kukosolewa na kuwaambia waandishi wa habari, kwamba yeye haamini katika kuwabana.

“Mimi siamini katika kuvibana vyombo vya habari, kwa sababu vyombo vya habari vinasaidia kuleta taarifa za maendeleo, vinafichua maovu yanayofanywa na baadhi ya watu serikalini na pia vinatoa mrejesho, vina habarisha na kuwaelimisha wananchi.

“... Kwa hiyo vyombo vya habari endeleeni kutukosoa, lakini mtukosoe kwa adabu kwa sababu

kuishi kistaarabu ni pamoja na kuwa huru kusikia mawazo ya wengine, ingawa simaanishi kukashifiana, kutukanana wala kukebehiana,” alionya Rais Samia.

Katika kauli yake ya pili, Rais Samia alivitaka vyombo hivyo viendane na kasi ya kukua kwa teknolojia kwa kuwa uzoefu unaonyesha vyombo vingi vya habari nchini, haviendani na kasi hiyo.

“...Vilevile eleweni kwamba, utoaji wa habari kwa sasa umehamia kwenye social media (mitandao ya kijamii), kwa hiyo, watu wa social media mjitahidi kuchuja habari zenu, kwani tukiandika mabaya ya nchi yetu, tutakuwa tunajichafua wenyewe,” alisema Rais Samia.

Baada ya kuyasema hayo, Rais Samia alitoa agizo lake la tatu katika sekta ya habari kwa kusema waandishi wa habari nchini wana jukumu la kutorarua nyuzi zinazounganisha kitambaa cha taifa.

“Msiingie kwenye mtego wa kurarua nyuzi zinazounganisha kitambaa cha taifa letu. Si mnakijua kitambaa cha taifa letu? Sasa msiende kuzifumua zile nyuzi, kile kitambaa kinatakiwa kiwe ‘strong’ (imara) ili kiendele kupepea.

“... Tafadhalini msiende kukifumua hicho kitambaa kwa sababu, najua nyie ni watu muhimu sana kwa usalama na utulivu wa taifa letu.

“... Vyombo vya habari mnatakiwa kuandika habari za kujenga wala siyo kubomoa. Kwa mfa-

Inaendelea Uk. 24

Uchambuzi**Nondo za Samia kwa vyombo vya habari****Inatoka Uk. 23**

no, katika kipindi hiki tunachoelekea kwenye uchaguzi, ndicho kipindi mnachotakiwa kueleza mazuri yaliyofanywa na vyama vya siasa na waelimisheni wananchi kuhusu haki zao za uchaguzi.

“... Msitoboe dau mnalosafiria, msiivue nguo nchi yetu utadhani mnacheza singeli. Hata kama kuna mabaya, kuna namna ya kuyaandika kwa sababu huko kwa wenzetu, nako hawafanyi hivyo katika nchi zao,” alisema Rais Samia.

Agizo lake la nne kwa vyombo vya habari alilielekeza kwa taasisi za serikali zinazodaiwa madeni na vyombo vya habari, ambapo alizitaka wizara zote na taasisi hizo, zilipe madeni hayo kabla ya mwisho wa Desemba mwaka huu.

“Hilo suala la madeni, nimekutana nalo mara nyingi, kuna madeni mengine yanalipika na mengine hayalipiki kwa sababu hayana ushahidi kutokana na ‘verification’ (uhakiki) tuliyofanya.

“... Kwa hiyo, taasisi na wizara zote zihakiki madeni yote ya vyombo vya habari ili yalipwe kabla ya mwisho wa Desemba mwaka huu. Madeni hayo yakishalipwa, na nyinyi wamiliki wa vyombo vya habari muwalipe maandishi wenu kwa sababu inaonekana hamuwalipi mishahara kwa wakati. “... Kumbe nyie (waandishi wa habari) ni sawa na mfinyazi hulia vigaeni, hamlipwi mishahara, lakini mko kimya. Serikali ikichelewa kuli pa mishahara mnaandika, yaani ya kwenu du, ya wenzenu midomo juu,” alitania Rais Samia.

Agizo lake la tano alilielekeza katika uandishi wa habari za vijijini kwa kuvitaka vyombo vya

habari kuandika kwa wingi habari za vijijini.

Kwa mujibu wa Rais Samia, wananchi wa vijijini wanahitaji kupata habari mbalimbali ili ziweze kuwasaidia katika suala la maendeleo.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alivitaka vyombo vya habari viwe na utaratibu wa kuwaalika viongozi mbalimbali ili wajadiliane kuhusu mambo mbalimbali yanayolihusu taifa.

Pia, Nape aligusia Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 na kusema baadhi ya vifungu ambavyo bado vinalalamikiwa na waandishi wa habari, vitaendelea kufanyiwa marekebisho kulingana na mazingira yatakavyoruhusu.

“Siwezi kutunga sheria kwa ajili ya kunyanyasa kwa sababu na mimi nina watoto ambao wanaweza kuwa wana habari.

“... Kwa hiyo, nikitunga sheria ya kuumiza, nitakuwa najiumiza mwenyewe siku mwanangu akiwa mwana habari. Sasa basi, naomba tuaminiane kuhusu sheria zetu, yanayowezezana, tutayafanya, yasiyowezezana tutasubiri wakati mwingine,” alisema Waziri Nape. Awali, mwenyekiti wa kamati ya kutathmini hali ya uchumi wa vyombo vya habari, Tido Mhando, alikabidhi ripoti ya kamati yake kwa Rais Samia na kueleza kwa kifupi hali ilivyo katika vyombo vya habari nchini.

Tido alisema kamati yake iliona kuna umuhimu wa serikali kuruhusu wawekezaji wa nje kumiliki asilimia 75 ya hisa katika vyombo vya habari vya ndani na wazawa wamiliki asilimia 25 kama njia ya kukaribisha mitaji ya kuboresha vyombo vya habari nchini.



Wadau mbalimbali wa sekta ya habari pamoja na baadhi ya mabalozi wakiwa kwenye kongamano hilo la habari. (Picha na Ikulu).



Mbunge Oran Njeza

Madeni ya wakandarasi yatisha Bunge

Na Mwandishi WETU,
Dodoma

SIFA ambazo serikali inajipatia kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali hazina maana sana kwani nyuma yake kuna madeni makubwa ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma nyingine ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu.

Hali hiyo imetisha Kamati ya Bunge ya Bajeti ambayo katika taarifa yake kuhusu bajeti ya mwaka 2024/25, imeitaka serikali kulipa malimbikizo hayo haraka.

“Pamoja na mafanikio hayo katika utekelezaji wa bajeti, Kamati imebaini kwamba kuna malimbikizo ya madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma ambayo hayajalipwa kwa kipindi cha muda mrefu,” inasomeka sehemu ya taarifa hiyo ya kamati iliwasilishwa bungeni wiki iliyo-pita na mwenyekiti wa kamati hiyo, Oran Njeza.

Kilichosikitisha kamati hiyo ni kuwa madeni mengi ni yale ya kujitakia, kwani mengine husababishwa na tabia ya maofisa masuuli kufanya ununuzi bila kuwa na fedha na wakati mwingine kuchelewa kufanya uhakiki wa hati za madai.

Aidha, kamati hiyo imebainisha kuwa kume-

kuwa na usimamizi usioridhisha wa miradi kulingana na matakwa mikataba.

“Kamati inashauri serikali kuja na mkakati madhubuti wa kulipa madeni ili kuondoa mkwamo uliopo katika utekelezaji wa miradi. Uli-paji wa madeni utaipunguzia serikali mzigo wa riba na adhabu zinazoambatana na madeni hayo, lakini pia utaongeza fedha katika uchumi, hivyo kuchochea ukuaji wa pato la taifa na kurejesha ukwasi kwenye uchumi,” inasema taarifa hiyo.

Aidha, Kamati imeitaka serikali kuachana na utaratibu wa kuanzisha miradi mipya wakati bado haijakamilisha miradi mingine.

Kamati imebainisha katika taarifa yake kuwa uchambuzi wake umebaini kwamba kuna miradi mingi ya sekta mbalimbali ambayo haijakamilika, lakini serikali inaanzisha miradi mingine mipya.

“Hali hii inasababisha serikali kuwa na mzigo mkubwa wa mahitaji ya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mipya na kukamilisha miradi ya zamani....

“... Hivyo, kamati inaishauri serikali kumaliza miradi ya zamani kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi mipya kama ilivyo kipaumbele cha bajeti ya mwaka 2024/25,” anasema Njeza.

Akiba ya serikali

Kuhusu akiba ya fedha za kigeni, kamati imeitaka serikali kuimarisha utaratibu wa Benki Kuu kununua dhahabu na kuihifadhi kama aki-ba ya taifa.

Kamati ilitoa ushauri huo kwa kuzingatia kuwa bei ya dhahabu duniani imeendelea kuwa juu na kufikia wastani wa dola za Marekani 1,952.4 kwa wakia mwaka 2023, ukilinganisha na dola za Marekani 1,727.3 kwa wakia mwaka 2022.

Hadi kufika Aprili, 2024 Benki Kuu imenunua dhahabu yenye thamani ya dola za Marekani milioni 26, katika lengo la kununua tani 6 za dhahabu yenye thamani ya dola za

Marekani Milioni 400.

Deni la serikali

Akizungumzia deni la serikali, mwenyekiti wa kamati hiyo alisema uchambuzi wa kamati imeonyesha kutishwa na ongezeko la deni hilo kwa asilimia 26.9 katika kipindi cha mwaka mmoja tu.

Inaendelea Uk. 26

Madeni ya wakandarasi yatisha Bunge

Inatoka Uk. 25

Njeza alibainisha kuwa hadi Aprili 2024, deni la serikali lilikuwa ni shilingi trilioni 91.71 ikilinganisha na shilingi trilioni 77.01 katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la shilingi trilioni 14.7.

“Pamoja na kwamba deni la serikali ni himilivu kwa

viwango vyote vya kimataifa, kamati inaendelea kuishauri

serikali kuweka mikakati ya kuonegza mauzo ya nje ili yatoe mchango mkubwa zaidi katika malipo ya deni la nje.

Kamati ilibainisha kuwa ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mauzo ya bidhaa nje umefikia asilimia 11.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 15.

Aidha, kamati ilionyesha wasiwasi wa kukua kwa deni lenye masharti ya kibiashara.

Hadi kufikia Machi 2024, deni lenye masharti ya kibiashara lilikuwa asilimia 60, kati yake asilimia 26.9 lilihodhiwa na benki za biashara za nje na asilimia 33.1 lilihodhiwa na asilimia 22 benki za biashara za ndani.

“Kamati inaishauri serikali kuhakikisha mikopo yenye masharti ya kibiashara ielekezwe katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati yenye sura ya kibiashara na yenye matokeo chanya pindi itakapokamilika mapato yake yasaidie kulipa

deni,” anasema Njeza.

Katika mwaka wa fedha unaomalizika, serikali ilitarajia kukopa shilingi trilioni 5.44 kutoka soko la ndani kwa masharti ya kibiashara ambapo hadi Aprili, 2024 jumla ya shilingi trilioni 4.61 zilikopwa sawa na asilimia 84.7 ya lengo.

Aidha, hadi kufika Machi, 2024, mikopo ya ndani ilikuwa imefikia asilimia 33.64 ya deni lote la serikali. “Kamati imebaini kuwa wakopeshaji wakubwa wa serikali ni benki za biashara zikifuatiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii ambapo hadi mwishoni mwa mwaka jana ilikuwa inamiliki asilimia 35.2 na 36.3 ya mikopo hiyo mtawalia,” anasema Njeza.

Kamati imebaini pia kwamba benki zinavutiwa zaidi kukopesha kwa ajili ya kutekeleza shughuli binafsi na siyo sekta za uzalishaji kama Kili-mo.

Kutokana na hilo kamati ikaishauri serikali kupunguza riba za mikopo kwa wafanyakazi kwa kuwa mikopo hiyo haina gharama kubwa na ina viwango vidogo vya viatarishi.

Kamati imebaini pia kuwa asilimia 78 ya Watanzania hawana akaunti za benki na kwa kiasi kikubwa hiyo inatokana na ukosefu wa elimu ya fedha, gharama za kumiliki na kuendesha akaunti za benki na uhaba wa upatikanaji wa huduma za kibenki katika baadhi ya maeneo hasa maeneo ya vijijini.



Kamati ya Bunge ya Ba-jeti na Uchumi ikikagua moja ya miradi mikubwa ya serikali.



Waziri Mkuu Mstaafu wa Kenya- Raila Odinga.

Raila bingwa wa siasa mwenye roho ya paka

Na Julius MKAMBI

SENETA wa Uasin Gishu nchini Kenya, Jackson Mandago, aliwahi kuwapa ushauri wanasiasa akiwataka waache kuweka siasa rohani na badala yake kuweka kwenye mapafu, akiwa na maana kuwa ukiweka kitu rohani, itadumu, ila kwenye mapafu, inatoka unapopumua.

Ni ushauri aliowapa kama njia ya kupunguza uhasama unaojitokeza mara kwa mara pindi uchaguzi unapokamilika, ambapo wapo wanasiasa, hususan wanaoshindwa hujaa hasira na kutengeneza chuki dhidi ya walioshinda.

Miongoni mwa wanasiasa ambao wameonyesha ukomavu baad aya kuzama na kuibuka upya kisiasa pindi uchaguzi mkuu unapokamilika, ni aliyekua Waziri Mkuu Raila Odinga.

Mara tano, Odinga amegombea urais na kushindwa ambapo kati ya hizo tano, alienda mahakamani mara tatu kupinga matokeo ya urais.

Na mara tatu, ni mara moja tu ambapo mahakama

iliamuru uchaguzi wa urais urudiwe, lakini Raila na kundi lake walisusia wakidai Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) haikufanya marakebisho kama ilivyoagizwa na mahakama.

Odinga ambaye baba yake mzazi, Jaramongi Oginga Odinga alikuwa Makamu wa Rais (wa kwanza), amejipatia umaarufu kisiasa akijivunia kuungwa mkono katika kila pembe ya nchi, ikiwemo ngome za upinzani.

Hata hivyo, nafasi ya urais ndiyo imekuwa ikimponyoka kila uchaguzi mkuu unapofanyik, huku akilalamika kuibiwa kura, matokeo yake kuitisha maandamano nchi nzima na hata kuna wakati alijiapisha kama 'Rais wa Wananchi.'

Licha ya Raila kuwapa wakati mgumu viongozi waliopo madarakani kutokana na kutekeleza majukumu yake kama kiongozi wa upinzani, amekuwa akifanikiwa 'kujipenyeza' serikalini jambo ambalo linawafanya wachambuzi kuona hatua hiyo inadhoofisha upinzani.

Katika uchaguzi mkuu uliyopita - 2022, Raila akiwania nafasi ya urais, huku akiungwa mkono na Rais Uhuru Kenyatta aliyekuwa anamaliza muda wake, alishindwa na William Ruto.

Inaendelea Uk. 28

Kenya

Raila bingwa wa siasa mwenye roho ya paka

Inatoka Uk. 27

Cheche za maneno zilirushwa baina ya viongozi hao wawili, lakini sasa wanaonekana kushirikiana, hususan baada ya Raila kutangaza nia yake ya kuwania uenyekiti wa Umoja wa Afrika.

Rais Ruto alitangaza kuongoza kampeni kuhakikisha Waziri Mkuu huyo wa zamani anamrithi Mousa Faki.

Aidha, baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2017, ulioshuhudia Raila akishindwa na Kenyatta kisha kujiapisha Rais wa Wananchi, alifanikiwa kujipenyeza serikalini katika tukio lililofahamika kama 'handshake' hivyo kutuliza joto la siasa.

Ukaribu wa Rais (mstaafu) Kenyatta na Raila, ulimiyima usingizi Ruto ambaye wakati huo alikuwa naibu rais hali iliyomlazimu kujipanga upya kutimiza ndoto yake ya kuwa Rais wa Kenya, akifahamu fika hana 'sapoti' ya Kenyatta.

Raila pia alifanikiwa kuingia serikalini baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007 uliogubikwa na machafuko. Hii ni baada ya kundi la watu mashuhuri akiwemo Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Benjamin Mkapa, kuwapatanisha Raila na Mwai Kibaki aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu Kenya na kufanikiwa kuunda serikali ya umoja wa kitaifa.

Vilevile baada ya uchaguzi wa mwaka 1997, akimaliza nafasi ya tatu nyuma ya Rais Daniel arap Moi, Raila ambaye alikuwa Mbunge wa Lang'ata, aliungana na chama tawala wakati huo na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nishati.

Raila amekuwa akicheza kwa umakini karata zake za kisiasa kutokana na namna anavyoweza kushirikiana na viongozi waliopo madarakani, wakati huohuo akiendelea kubakia kama kiongozi wa upinzani, hivyo kuwachanganya wanasiasa waliyopo serikalini na wenzao wa upinzani.

Mara zote Raila anaposhirikiana na rais aliyopo

madarakani tafsiri yake ni kuwa anasaka kuungwa mkono atakapowania urais uchaguzi unaofuata, lakini mambo yamekuwa yakiende kinyume na matarajio yake na hata wafuasi wake ambao kuna wakati wanakaribia kukata tama wakieleza kuwa "anawachezea shere."

Kwamba Raila anatumia mgongo wa kuungwa mkono na kupata kura nyingi wakati wa uchaguzi, huku akijua kuwa ahata akishindwa, atakuwa na uhakika wa mkate wake na familia ya Odinga kuisi vyema.

Hoja hii wachambuzi wa siasa wamekuwa wakiipinga kama ambavyo Raila amekuwa akifanya, huku ikielezwa kwamba kiongozi huyo hushindwa kwa "mbinu tu za kuhesabu kura na kuzidiwa maarifa na wapinzani wake."

Hata hivyo, bado yapo matumaini kwa Raila mwenyewe na mashabiki wake kuwa uchaguzi ujao wa 2026, ana nafasi ya "kupindua meza" ili angalau aongoze Kenya kwa muhula mmoja na kutimiza ndoto yake ya kuongoza taifa hilo la Afrika Mashariki lenye uchumi imara zaidi ya majirani zake.



Rais wa Kenya - William Ruto.

Ni wakati wa kuwapa wanachama dhamana...

Inatoka Uk. 30

kongwe nchini kuanza kutumia njia ya kiasa kuajili wanachama wake. Hivi aa wanachama wa Yanga wanandikihwa kidijiti kupitia njia mbalimbali kama vile kujiunga moja kwa moja klabuni, kwa kutumia N-Card au kupitia akaunti za benki.

Kwa kipindi kifupi cha kuanza kutumika kwa utaratibu huo uanachama umegeuka kuwa moja na njia kubwa za kuiingizia klabu mapato tofauti na zamani ambapo waliokuwa wanatamba ni mahabiki ambao hawakuwa na mchango mkubwa kifedha kwa klabu.

Miezi kadhaa iliyopita imba iliwahi kupewa tuzo ya mahabiki bora na hirikiho la oka Afrika (CAF) kutokana jini walivyoonyeha kuinga mkononi klabu yao wakati ikihiriki katika mahindano ya kimataifa.

Hii yote inaonyeha umuhimu wa wanachama katika uendehaji wa klabu. Hivi aa wanachama i muhimu tu katika kuweka hamaa kwa kuhabikia wakati wa mechi, bali nao ni chanzo kimoja kikubwa cha mapato kwa klabu.

Pamoja na kulipa kiingilio lakini inatarajiwa pia wanachama ndio watakuwa wateja wakubwa wa bidhaa zinazozaliwa na klabu kama vile jezi, fulana nyinginezo, kafu na bidhaa nyingine zenye nembo ya klabu. Kwa maana hiyo wakati wa kuwona mahabiki ni muhimu tu kwa kuihangila klabu zimepitwa na wakati. Hivi aa uendehaji wa klabu unataka kuwageuza mahabiki kuwa wanachama ambao katika mabadiliko ya uendehaji yanayofanywa na klabu hapa nchini nao watakuwa ehemu ya umiliki wa klabu hizo.

Tumeona mfano wa mabadiliko yanayofanywa na Yanga na imba wanachama ndio wamiliki wakubwa wa klabu hizo wakiwa na ailimia 51 ya hia zote za klabu huku wawekezaji wakitengewa ailimia 49 ya hia.

Hii ina maana kuwa hata viongozi wa klabu hizi wanatakiwa kubadili mtazamo wao kuhuu mahabiki na wanachama. Hivi aa wanachama wanapawa kupewa nafai yao ndani ya klabu kama ehemu ya wamiliki.



Wanachama wa Yanga wakiwa kwenye mkutano mkuu.

Kile kipindi ambacho viongozi ndani ya klabu ndio wanajiona kuwa ni wao ndio mwanzo na mwiho kimepitwa na wakati.

Viongozi wajidanganye kuwa fedha za wafadhili peke yake zitaweza kuendeha klabu kwa ufanii. Ni kweli mfadhili anaweza kutoa kiai kikubwa cha fedha ambazo zitatumika kununua wachezaji bora na kutengeneza miundombinu ya timu. Lakini timu hiyo iipokuwa na uungwaji mkono miongoni mwa mahabiki na wanachama bai hiyo yote inaweza kuwa kazi bure.

Zipo timu ambazo zimewahi kuyumba kifedha lakini zikaendelea kuwa imara kiwanjani kutokana na kuwa na mingi mkubwa wa kuungwa mkono na mahabiki, tena wakati huo hata kabla ya mfumo wa wanachama haijawa na mizizi katika klabu zetu.

Mahabiki wa timu hizi nao wanapawa kufahamu kuwa wakati wa wao kujibadili kuwa wanachama ndio huu. Kuna faida kubwa ya kujiongeza kutoka kuwa habiki na kuwa mwanachama.

Kama mahabiki wanataka kuwa na auti kubwa ndani ya klabu bai wanapawa kuwa wanachama rami. Ukiwa mwanachama bado utakuwa na nafai ya kuihangilia timu yako lakini pia kuiwezeha kimapato na hivyo kukupa auti katika mauala ya uendehaji wa klabu.

Ukiwa habiki utabakia kuwa mtu wa kupiga kelele tu kwenye kuhangilia lakini hautakuwa na auti katika uamuzi wa muala muhimu yanayohuu klabu.

MICHEZO

Jumatatu, Juni 24-30, 2024



Rais wa Yanga SC, Injini Hersi Said (kushoto), akiwa na Mwenyekiti wa Simba SC, Murtaza Mangungu.

Ni wakati wa kuwapa wanachama dhamana kuongoza vilabu

Na Mwandishi Wetu

Majuzi hapa tulihuhudia mahabiki wawili maarufu wa kluba ya imba wakifungiwa kujihuiha na hughuli zozote za kluba kutoa na kile kilichodaiwa kuitiha mkutano wa wanachama kinyume na taratibu.

Kabla ya hapo kuna mwanachama mwingine

maarufu wa kluba hiyo hiyo aliwahi kukamatwa na kuwekwa mahabuu kwa iku kadha kwa tuhuma za kutihia ualama na kuhatarisha amani kutokana na matamhi yake.

Wakati hayo yakitokea viongozi wa kluba hiyo pamoja na kluba nyingine kuba nchini wamekuwa wakihangaika kutafuta uungwaji mkono kwa kuhawihi watu wajiunge na kluba hizo kama wanachama.

Juzi juzi wakati Yanga ikifanya mkutano wake mkuu ilitangaza kuwa mwaka uliopita imeingiza kiai cha hilingi milioni 6 kama ada zilizolipwa na wanachama wapya aliojiunga na kluba hiyo.

Fedha hizi zimepatikana baada ya kluba hiyo

Inaendelea Uk. 29

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

